Jina ……..…… Namba Yako…….

Sahihi ya mtahiniwa ……..

Tarehe……..

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
Julai/Agosti 2013
Muda:
Saa 2 $^{1}/_{2}$

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA WESTLANDS

HATI YA KUHITIMU KISOMO CHA SECONDARL KENYA

KISWAHILI'
Jalai/Agosti
Muda: Saa ***2 $^{1}/_{2}$***

MAAGIZO

a) Andika jina iako na namba yako katika nafasi uiizoachiwa hapo juu.

b) Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu,

c) Jibu maswali yote.

d) Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kujitabu hiki cha maswali.

KWA KAZI YA MTAHINI

Swali	Sehemu	Upeo	Alama
1	Ufahamu	15	
2	Ufupisho	15	
3	Matumizi ya lugha	40	
4	Isimu Jamii	10	
Jumla		80	

SWALI LA KWANZA: UFAHAMU

Sotna taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Ni dhahiri shahiri kwamba ***uharamia*** umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili Jimeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika Mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kiiripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yumkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suaia hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawa na ulipuaji wa bomu mjini Nairobi na Dar-es salaam mnamo Agosti 7, 1998, na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marelcani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno Icwa maliaramia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukoselu wa tawala-wajibika katika rnaeneo kunakotokea unyama huu ni ihibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuehipuka kwa janga hili. ’

Mchipuko wa baa la uharamia umelenga jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umasikini na magonjwa yaliyosheheni pakufiwa barani. Bila shaka, hili ni suaia linalosgwirishwa na ***‘kinyume mbele’.*** Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiri'a na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.
. Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kuzipiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawaia wa nchi kunakochipuka uharamia haujazatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo ya malengo ya maendeleo ya millennia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo na upanuzi wa masomo ulimwenguni. Hg^akati za kitalii katika kanda mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Ni muhali kwa utalii kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. Itakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za ***mtandao*** ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu vfa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwa hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kandaya mwambao zimetiliwa shaka si haba. Itabidi milcakati kabambe na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa. ~

MASWALI

Kwa mujibu wa taarifa uharamia ni nini? **(aiama 2)**

Tatizo la uharamia linamotishwa na nini? **(aiama 2)**

c) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwengu? (aiama 2)

d) Fafanua dhana ya “kinyume mbele” kwa mujibu wa taarifa hii. (aiama 2)

e) Uharamia uriaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua. (aiama 2)

f) Thibitisha kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia. (aiama 2)

g) Eleza maana ya msamiati hull jinsi ulivyotumiwa katika kifungu hilci. (aiama 3)

I) azma

51) mtandao

iii)Kuzipiga jeki

UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Dawa-^a kulevya zinaweza kugawika katika makundi mawili makuu; dawa hasi na dawa sugu.
Katika kundi la kwanza zinaingia dawa zozote ambazo hunywewa, hunuswa au hutumiwa kwa nia ya kulevya au kumwingiza mtumiaji katika hali ya kujihisi amepanda. Dawa za aina hii huwa na matokeo hasi kwenye mwili wa mtumiaji. Inawezekana jamii itakubali kuwepo kwake, pamoja na kutumiwa kwake, lakini, matumizi ya kipindi kirefu huwa na matokeo mabaya sana kwa watumiaji. Baadhi ya dawa hizi ni bidhaa za tumbaku ambazo huwa na aina za kemikali inayoitwa nikotini. Nyingine ni vileo kama wiski, bia, divai, miraa au mairungi, gundi ya viatu na bidhaa zinazotokana na petroli.

Hebu sasa tuangalie zile zinazoitwa dawa sugu. Hizi ni dawa ambazo kimsingi humchangamsha mtumiaji na kumfanya apandwe na nishati za ajabu. Dawa hizi hufanya hivi kwa kuzitekenya seli za ubongo wa anayehusika. Katika kulifanya hili dawa zenyewe huishia kuzuia seli za ubongo huo.
Huu ndio msingi wa mtumiaji kuwa na ustahimilivu fulani wa dawa zenyewe. Ustahimilivu huu ndio unaomfanya awe kama aliyetawaliwa na dawa hizo. Yaani matumiaj i huwa hana njia nyingine ya kujizuia na huishia kuwa mtumwa wa dawa hizo. Baadhi ya dawa sugu ni bangi, afyuni, heroini, mihadarati na kokeini Baadhi ya wataalamu wanajumlisha miraa katika kundi hili pia.

Ni kawaida kusikia madai kuwa mtu anayetumia dawa za kulevya huonekana kuwa na furaha kuliko wenzake. Ili kuelewa chanzo cha msisimko na furaha hiyo ya ajabu, lazima tuzijue hatua anazopitia mtumiaji dawa za kulevya. Kimsingi kuna hatua tatu kuu. Mara tu mtu anapozitumia ' dawa za kulevya, dawa hizo huzichangamsha seli za ubongo kwa kiasi kikubwa. Kuchangamshwa huku kwa seli kunazuia mwili wa anayohusika kutopata hisia kutoka viungo vya mwili au misuli ya mwili. Matokeo ya hali hii ni kumfanya mtu anayehusika kutenda mambo kupita kawaida, anaweza kucheza kwa kipindi kirefu na kadhalika. Hali hii inaweza kuitwa hali ya ‘mpumbazo’. Mpumbazo huu unaweza kumdanganya anayehusika kuhisi kuwa ana uwezo usiokuwa wa kawaida. Lakinii hii ni hali ya muda tu ambayo hutangulia kuuliwa na kuharibiwa kwa seli za ubongo.

Mtumiaji anayeingia katika hatua ya pili huwa anatoka kwenye ile hali ya mpumbazo. Hatua ya pili hutambulishwa na dalili zifuatazo: Uchovu, kulala kupita kiasi, kutokuwa na hamu ya kazi au mambo mengine. Kupuuza maswali ya siha na afya, usahaulifu, kukosa malengo au shabaha katika kazi yake, kupungukiwa na kumbukumbu, kujitenga na watu wengine na kuwa na hisia za chuki au uhasama na jamaa. Mtumiaji anapofikia hatua hii hutambulikana waziwazi na watu walio karibu. Mtumiaji wa dawa za kulevya huweza tu kunusurika au kuokolewa katika hatua hii. Akipita hatua hii ya pili, huwa anaingia katika awamu mbaya sana.

Hatua ya tatu ya mtumiaji wa dawa za kulevya huitwa hatua ‘isiyo ya kawaida’. Sifa za kutambulisha mtumiaji aliye kwenye ngazi hii ni fadhaa kubwa, unyonge wa mwili umbu wa kimawazo na uvunjifu mkubwa. Mtumiaji aliyefikia ngazi hii huonyesha sifa kadha milele.
Mathalani kujitenga kabisa na jamaa au watu walio karibu naye, kupaliwa kabisa na usingizi, kuudhika haraka na kuwa na tabia ya kuonyesha uchukivu wa vitu kwa kupigana, kuchanganyikiwa kunakotokana na kuharibikiwa kwa seli za ubongo, wazimu au kuangukaanguka kama mgonjwa wa kifafa. Katika ngazi hii, seli za ubongo zinazomsaidia mtu kufanya uamuzi mzuri huwa zimeharibiwa na dawa zenyewe. Si ajabu basi kuwa mtumiaji anaonyesha tabia za kitoto na huishi kama mtu aliye kwenye ndoto. Hatimaye ubongo unazongwa kabisa kutokana na madhara ya seli na mtumiaji huweza kushikwa na magonjwa ya kiakili kama wendawazimu.

Mwisho wa mtumiaji wa dawa za kulevya aliyefikia ngazi hii ni kufariki baada ya mwili wake kushindwa kuhimili uzito wa dawa zenyewe. Wengine huishia kujinyonga au kufariki kutokana na* madhara ya moyo.

MASWALI

a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili. (Maneno 70)
(aiama 9)

Jaribio

Jibu

b) Eleza hatua anazopitia mtumiaji wa dawa za kulevya (Maneno 60) (aiama 6)

Jaribio

3. MATUMIZI YALUGHA

I) Sahihisha sentensi ifuatayo: (aiama 2)
Maziwa hii ilinunuliwa jumamosi.

II) Tunga sentensi ukitumia kitenzi ‘choma’ katika kauli ya kutendua. (aiama 2)

iij) Taja sifa mbili za sauti /na/. (aiama 2)

iv) Unganisha sentenzi zifuatazo kwa kutumia kirejeshi cha kati ipasavyo.

Jembe-Iimepotea. Jembe ni ietu. (al&ma 2)

v) Changanua sentensi iftiatayo kwa mehQ.ro wa visanduku. (aiama 4)
Wataiii wengi wataenda Mombasa mwakani.. >' .

*

vi) Ainjsha vishazi katika sentensi iftiatayo: (aiama 2)

Bondia aijyesMnda pigaao jaaa aiituzwa zawadi kemkem.

vii) IZIeza tofauti kati ya: a) Ningalirauka rfiapema ningalimwahi. **(aiama 2)**

b) Ningerauka mapema ningemwahi. **(aiama 2)**

viii) Ainisha viambishi: • **(alama2)**
Walisaidiana

ix) Bainisha shamirisho katika sentensi iftiatayo; **(aiama 3)**
Mama alimsafirishia mtoto wake nguo kwa gari iajirani.

x) Tumi a neno 'shujaa' katika sentensi kama; **(aiama 2)**

a) Kielezi

b) Kivumishi

xi) Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo kudhihirisha ngeli. **(aiama 2)**

a) Maiti

b). Jua :

xii) Yakinisha sentensi ifuatayo; **(aiama 2)**
Sitaenda Entebbe mwakani

xii!) Unda nomino kutoka&%pa kitenzi‘vuka’ **(aiama 1)**

xiv)EIeza matumizi ya 'po' katika sentensi ifuatayo. **(aiama 2)**
Mkurugenzi alipofika alielekea walipokuwa wageni waheshima.

xv) Andika katika wingi: (aiama 2)

Mwanamiehezo mwingine ameondoka nchini kujiunga na yule aliyeondoka wiki jana.

xvi)Andika katika udogo; ^

Mtu huyu atanunua shamba. (aiama 2)

xvii)Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kiashiria cha kusisitiza cha karibu. (aiama 2)

Sisi tutalala ukumbini

xvili) Onyesha chagizo katika sentensi ifuatayo;

Wachuna chai walifanya kazi hiyo kwa uvivu mwingi ajabu. (aiama 2)

xix)Tumia neno ‘susa’ mara mbili katika sentensi moja kudhihirishamaana tofauti. (aiama 2);

4. ISIMU JAMII

Eleza maana ya dhana zifuatazo. (aiama 10)

a) Sajili

b) Kaida

c) Lugha

d) Lahaja

e) Uwili lugha